systems play

FARAHASHA KWA MVUMBUZI WA MIFUMO

AMALI

Ni kutumia nadharia katika matendo. Merriam-Webster Dictionary.

Ni makutano ya kujifunza na utendaji, na humaanisha kuyakutanisha haya mawili mara kwa mara, na kwa maingiliano ya kujirudia.

CHOMOZA

"Tendo la kuweka wazi tajriba za ndani za wafanyakazi wa shirika katika harakati ya kazi ya kila siku … mawazo na hisia, matamanio na hofu, thamani na kumbukumbu."

Social Innovation from the Inside Out, Warren Nilsson.

FIKIRA CHANGAMANO

Kwa sababu ya asili ya uchangamano na mahusiano baina ya mamlaka na muundo vilivyo fafanuliwa hapo juu, hatuwezi kujifikiria kuwa nje ya mfumo. Hatutarajii mambo kujiendesha yatakavyo na tunaporudia kufanya jambo hatulitarajii kuwa sawa mara ya pili.

Fikira changamano hutumia ufahamu wetu wa mifumo changamano ya kawaida katika mielekeo yetu ya uvumbuzi wa kijamii—na katika mchakato wenye nguvu wa mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kiufundi, na kitamaduni ambayo yatakuwa sehemu ya mabadiliko ya kimfumo.

FIKIRA ZA KIMIFUMO

Tapo la kimafikira ambalo linalenga kutambua maingiliano baina ya sehemu za mfumo na kuyachunguza katika muungano wa kitu kimoja kizima.

The Vocabulary of Systems Thinking: A Pocket Guide, na Colleen Lannon.

FIKIRA-TATUZI

Mbinu ya fikira-tatuzi—mara nyingi ikiitwa tu fikira-tatuzi—ni mwelekeo wa utatuzi wa shida, kujifunza, au ugunduzi ambao hutumia njia tendaji ambayo si hakika kwamba ni toshelevu au inafaa, lakini inatosha katika malengo ya wakati huo.

Wikipedia.

Katika mazungumzo ya kawaida, huwa tunaichukulia fikira-tatuzi kama mawazo ya njia mkato ambayo hutuwezesha kutatua shida na kufanya maamuzi ya haraka na kwa ufanisi. Fikira-tatuzi husaidia katika hali nyingi lakini pia huweza kusababisha mapendeleo ya kimawazo.

Very Well Mind, Kendra Cherry.

HATUA YA MAAFA

Ni hatua muhimu katika hali fulani, mchakato, au mfumo ambapo zaidi yake athari au mabadiliko, ambayo mara nyingi hayazuiliki, hutokea.

Merriam-Webster Dictionary.

Mifumo ya ikolojia-jamii mara nyingi huwa haiathiriki kulingana na kuongezeka au kupungua kwa shinikizo, na pindi tu zipitapo kiwango fulani, au hatua ya maafa, ongezeko lolote la shinikizo linaweza kuanzisha ghafla mabadiliko makubwa na ya kasi ambayo hayawezi kurekebishwa kwa urahisi. Pindi hatua ya maafa ipitwapo, mfumo unaweza kuingia katika hali tofauti au kufuata mkondo tofauti wa maendeleo.

Tazama Catastrophic shifts in ecosystems, Scheffer, na wengine na Regime shifts in the anthropocene: drivers, risks, and resilience, Rocha na wengine.

HATUA ZA UPANUZI

Donnella Meadows anafafanua hatua za upanuzi kama "Sehemu za kuingilia kati katika mfumo" kutengeneza mageuzi au mabadiliko katika mfumo. Alitambua tisa ya hatua hizo za marekebishi (zimeorodheshwa hapa chini kulingana na kushuka kwa ufanisi wake, kulingana na Meadows):

1. Mawazo au mtazamo ambamo mfumo ulitokana (malengo, miundo ya utawala, sheria, utamaduni).
2. Malengo ya mfumo.
3. Msambao wa mamlaka juu ya sheria za mfumo.
4. Sheria za mfumo (motisha, adhabu, vikwazo).
5. Msambao wa taarifa.
6. Msambao wa rasilimali na maingiliano ya raslimali.
7. Kuongoza mipindo ya majibu chanya.
8. Kudhibiti mipindo ya majibu chanya.
1. Vikwazo, mipaka, nambari (ruzuku, ushuru, viwango).

KAIDA

Imani na desturi ambazo hubaini uwanja wa tatizo fulani, na kuliongeza katika mapitio ya kila siku ya watu katika uwanja huo (kijamii, kiuchumi, kisiasa, nk.).

Ni neno linalotokana na sosholojia ambalo hufafanua "ruwaza thabiti za tabia ambazo hufasili, huongoza na kudhibiti tendo."

Oxford Bibliographies.

KUENEZA

Neno kueneza hutumika mara kwa mara kurejelea kueneza wazo kwa mafanikio. Hata hivyo, katika uvumbuzi wa kimifumo, tunabainisha aina tatu:

Kueneza kwenda nje: Ni kurudia au kunakili uvumbuzi katika ngazi moja (kawaida katika ngazi ya chini), kama vile kurudia programu iliyofanikiwa katika shule kadhaa, au hospitali kadhaa.

Kueneza kwenda juu: kubadilisah sheria, sera, kanuni (miundo ya viwango vya kati). Mara nyingi, uvumbuzi katika ngazi hii ni tofauti na uvumbuzi ambao umeenezwa kwenda nje kwa mafanikio katika ngazi ya chini.

Kueneza kwenda ndani: kubadilisha mahusiano, thamani, kaida, au imani, na kiwango cha ngazi ya jumla.

Mengi, tazama Scaling Out, Scaling Up, Scaling Deep: Advancing Systemic Social Innovation and the Learning Process to Support It, Darcy Riddell na Michele-Lee Moore.

KUIBUKA

Tabia ya vipengele na maingiliano ndani ya mifumo changamano ya kawaida kuunda ruwaza na utaratibu wa kitabia.

Uchangamano wa kiwango cha juu utokeao kutokana na vurugu ambamo miundo mipya, madhubuti huungana kupitia maingiliano miongoni mwa vitu anuwai ndani ya mfumo.

What is Emergence? Peggy Holman.

MABADILIKO YA MIFUMO *(wakati fulani huitwa uvumbuzi wa mifumo au mageuzi ya mifumo)*

Kimsingi, na kwa kiasi kikubwa, ni kubadili namna wengi wa wahusika muhimu wanatatua changamoto kubwa ya kijamii kiasi kwamba watu wengi wanaoathirika na tatizo hilo wanafaidika pakubwa.

Beyond Organizational Scale: How Social Entrepreneurs Create System Change, Martin Fisher.

Mabadiliko ya mifumo huhusisha kubadilisha viungo na maingiliano yajengayo mihimili ya mfumo—kanuni na viwango ambayo hufanya mfumo kufanya kazi jinsi unavyofanya kazi, na vile vile malengo, kaida na imani ambazo, ikiwa hazitakabiliwa, zitazuia mifumo kufanya kazi kwa njia jumuishi zaidi. “Yanahusisha mageuzi ya kina ya picha za akilini, mahusiano, na njia za utendaji kazi zinazopuuzwa almradi tu mabadiliko haya yanahusisha mageuzi katika majukumu ya mashirika na miundo rasmi, usimamizi wa vipimo na utendaji, na malengo na sera.

Academy for Systems Change, What Is Systems Change?

MAMLAKA

Uwezo wa mtu binafsi au kundi la watu kufanya kazi ndani ya mfumo.

Kuna mjadala kuhusu majukumu ya utendaji na muundo ndani ya mfumo na namna vinaingiliana. Je, muundo unakwamisha au kuimarisha utendaji? Je, utendaji unajenga na kuzalisha miundo? Au muundo na utendaji vinajijenga mizunguko ya mara kwa mara ya majibu?

What is agency? American Journal of Sociology, Emirbayer, M and Mische, A.

MATOKEO YASIYOKUSUDIWA

Kwa sababu ya kutokuwa moja kwa moja na kutotabirika, daima kutakuwepo na matokeo yasiyokusudiwa.

MATOKEO YASIYOTABIRIKA

Kwa ajili ya asili ya uchangamano, hatuwezi kutarajia mambo kuwa ya kutabirika na tunaporudia tendo hatuwezi kutarajia matokeo yawe sawa mara ya Pili.

MAUMBOASILI YA MIFUMO

Maumboasili ya mifumo yanaweza kuchukuliwa kama msuko jadi wa hadithi katika mfumo—ruwaza za kawaida na miundo ambayo hutokea mara kwa mara (Colleen Lannon). Miundoasili ni vifaa muhimu katika kutusaidia kujibu swali: "Kwa nini tunashuhudia matatizo yale yale yakijirudia kila wakati?" (William Braun). Kujifunza kuhusu maumboasili ya mifumo, tazama makala ya Braun 2002, The System Archetypes.

MCHORO WA MPINDO SABABISHI

Mpindo funge wa muungano wa usababishi na athari ambao huonyesha namna vipengele katika mfumo huingiliana.

The Vocabulary of Systems Thinking: A Pocket Guide, na Colleen Lannon.

MCHORO WA MPINDO SABABISHI: MPINDO SAWAZISHI

Mchakato sawazishi hutafuta ulinganifu—hujaribu kuleta vitu katika hali inayotakiwa na kuviacha hapo. Aidha hudhibiti na kuzuia. Mpindo sawazishi husawiri mchakato wa kulinganisha. Pia huitwa mpindo hasi.

MCHORO WA MPINDO SABABISHI: MPINDO WA KUIMARISHA

Michakato ya kuimarisha hutoa vyote ukuaji na kudorora—huchanganya mabadiliko kwa upande mmoja na na hata mabadiliko zaidi. Mpindo wa kuimarisha husawiri mchakato wa kuimarisha. Aidha unajulikana kama mzunguko mbaya au mzunguko mzuri na mpindo wa majibu chanya.

The Vocabulary of Systems Thinking: A Pocket Guide, na Colleen Lannon.

MCHORO WA MPINDO SABABISHI: MPINDO WA MAJIBU

Urudishaji wa majibu kuhusu hali ya mchakato. Kwa mfano, uchunguzi wa utendaji kazi wa kila mwaka ni njia ya kumrudishia taarifa mwajiriwa kuhusu hali ya kazi yake

The Vocabulary of Systems Thinking: A Pocket Guide, na Colleen Lannon.

MFUMO

Ni kundi la vipengele vinavyoingiliana, vinavyohusiana, au kutegemeana ili kuunda kitu kizima changamano. Kila mara hufafanuliwa kwa kuzingatia kusudi mahususi. Maneno mfumo na muundo wakati fulani hutumiwa kwa kubadilishana.

The Vocabulary of Systems Thinking: A Pocket Guide, na Colleen Lannon.

MFUMO FUNGE NA MIFUMO WAZI

Mifumo wazi huathiriwa na mazingira yake ilhali mifumo funge imejitenga na mazingira yake. Tofauti katika mipaka ya mifumo au jinsi imefafanuliwa inaweza kuamua ikiwa mifumo iainishwe kama wazi au funge.

MFUMO-IKOLOJIA

Ni mfumo au kundi la elementi zinazoingiliana, unaoundwa na maingiliano ya jamii ya viumbe katika mazingira; Mfumo au mtandao wowote wa sehemu zinazoingiana, kama vile katika biashara.

Dictionary.com

MIANYA YA KIMIUNDO

Various kinds of processes that occur in the spaces and cracks within some dominant social structure of power.

Envisioning Real Utopias, Erik Olin Wright.

MIFUMO CHANGAMANO YA KAWAIDA

Ni Mifumo inayobadilika na isiyo na maingiliano ya moja kwa moja. mifumo hii hujifunza yenyewe, hujiongoza, na hujizalisha.

Schwab Foundation, Social entrepreneurs and systems change, 2017.

Ni mifumo inayobadilika na inayojinufaisha, yenye utendaji katika kila kiwango, yenye sifa za dharura, inayodumu mbioni tayari kuingia katika uwezekano utokeao. Wanadamu, jamii, na mifumo-ikolojia ni mifano ya mifumo changamano ya kawaida

Triarchy Press.

MIPAKA YA MFUMO

Kubainisha mipaka ya mfumo ni muhimu ili kuifahamu mfumo. Mipaka mbalimbali huweza kutoa uchanganuzi na matokeo tofauti tofauti. Mipaka ya mfumo yaweza kuwa hatua muhimu ya mjadala wakati wa kuchanganua mifumo.

Schwab Foundation, Social entrepreneurs and systems change, 2017.

MITANDAO TULI

Mitandao tuli hufanya kazi kando na, lakini hupatikana sambamba na mitandao inayopatikana katika mifumo iliyokita. Mitandao hii inapambanuliwa na:

- Uhuru wa kisiasa na kuwa nje ya mivutano ya udhibiti na utekelezaji.
- Kuwa katika nafasi za kuunda sera *mbadala* (viangulio), kudiriki kujifunza kutokana na wenza, na kufikiri kubuni jinsi ya kutatua shida za rasilimali.
- Kuwa na uwezo wa kuungana na ulingo *rasmi* wa kisiasa na mitandao katika viwango mbalimbali.

Per Olsson, Research on Innovation and Transformation for People and Planet

MIUNDO

Ni asasi kaida zinazochonga na kudhibiti fursa za matendo ya kundi la watu au mtu binafsi.

Upo mjadala kuhusu majukumu ya mamlaka na na muundo kwenye mfumo na namna haya mawili yanaingiliana—swali kuu likiwa: ni utendaji huru kiasi gani mtu binafsi anaweza kuwa nao kwenye mfumo?

mf. Structure and agency, Wikipedia.

MIVUTO

Ruwaza ambazo mfumo hutuama. Almradi mipaka haijabadilishwa, mfumo ukipita karibu na mvuto, basi mfumo hautatoka eneo hilo. (Port na Van Gelder, uk. 573). Mfano rahisi ni kituo cha mvuto, kama vile kituo cha chini zaidi cha bembea.

MJANJA/UJANJA

Katika ngano, mjanja huwa na maarifa maalum na huvunja kaida mienendo ili kufichua thamani zilizofichika na kukabiliana na hali iliyopo. Katika ngano za Wamarekani-Wahindi, kwa mfano, mbweha huwa ndiye mjanja, akivuruga hali ya kawaida ya mambo na kukiuka mipaka. Katika mageuzi ya kijamii, ujanja ni elementi muhimu na ya lazima ili njia mpya zikafikiriwe kwa nia ya majaribio.

MJASIRIAMALI/ UJASIRIAMALI WA KIJAMII

Wajasiriamali wa kijamii wana ujuzi wa kutengeneza na kuanzisha mawazo, michakato na bidhaa mpya katika mfumo uliopo. Wengi hawagombani na asasi zilizopo (sheria, sera, uchumi, utamaduni), ila badala yake, husaidi kuendeleza ustahimilivu kwa kutoa nafasi ya kuzoe na kujifunza. "Wakati ambapo ujasiriamali wa kijamii unamlenga mtu binafsi na biashara ya kijamii kulenga mashirika, uvumbuzi wa kijamii unapania kubadili jinsi mfumo unafanya kazi." (Westley na Antadze). Mchoro huu unaonyesha tofauti miongoni….



Making a Difference: Strategies for Scaling Social Innovation for Greater Impact, Frances Westley na Nino Antadze.

MJASIRIAMALI/ UJASIRIAMALI WA MIFUMO *(wakati fulani ukiitwa mjasiriamali/ ujasiriamali wa kiasasi; pia tunatumia jina mvumbuzi wa mifumo)*

Kinyume na mjasiriamali wa kijamii, lengo la mjasiriamali wa mifumo—mvumbuzi wa mifumo —ni kuweka mabadiliko katika mfumo mzima (ngazi za chini, kati, na jumla)—yaani, si kusaidia mfumo uzoee, bali kuusaidia ubadilike. Hili huhusisha kuanzisha uvumbuzi wa kijamii, kuukita katika sheria, sera, au kanuni kuathiri mpangilio wa kijamii, na vile vile kubadilisha ruwaza za kawaida za kanuni, imani, mpangilio wa mamlaka na msambao wa raslimali za kijamii mambo ambayo mwanzo huchangia kuwepo kwa tatizo.

Kazi hii itahusisha kufahamu na kuweza kuchanganua na kukabiliana na mageuzi ya mifumo; kufanya kazi katika ngazi zote (nje, juu, na ndani); kupenyeza ngazi zilizosukana; na kulinganisha fursa katika mfumo na juhudi za mageuzi.

Surmountable Chasms: Networks and Social Innovation for Resilient Systems, Moore na Westley na The Evolution of Social Innovation, Per Olsson.

MKWATUZI

Mtu anayejishughulisha na ukwatuji—mojawapo ya majukumu ya mvumbuzi wa kijamii na mifumo.

MTANZIKO

Kuwa katika hali ya mtanziko ni kutoweza kuamua ni kipi ufanye kati ya vitu viwili kwa sababu kila kimoja chaweza kuwa na matokeo mabaya. Cambridge Dictionary.

Katika mifumo ya kijamii, matatizo mengi (kukosa makazi, umasikini, maendeleo ya miji) yana utata au ukinzani, hali iitwayo mitanziko wakati fulani. Kwa mfano, tunaweza kuhisi kwamba kila mtu anafaa kuwa na makao sawia na kuthamini mali ya mtu binafsi. Kuna utata mwingi katika jamii za wanadamu—km. mtu binafsi dhidi ya watu kwa pamoja; thamani ya wataalamu dhidi umuhimu wa kujisaidia. Tunaelekea kuzingatia upande mmoja wa mtanziko, tukifasili mmoja kuwa mzuri na ule wa pili mbaya, au kupendelea mmoja… Hata hivyo, uvumbuzi husisimka tunapofasili pande zote kwa misingi ya uzuri wake (km. sheria zenye haki *na* mahusiano ya kibinafsi; mali ya watu binafsi *na* makazi kwa watu wote, uchaguzi binafsi *na* majadiliano ya kutegemewa katika maslahi ya kijamii). Kwa ajili hii, maswali maovu ni bora yaulizwe kama utata unaohitaji upatanisho wa pande mbili kinzani, zote zikichukulia kuwa za faida.

Tazama Charting the Corporate Mind, Charles Hampden-Turner.

MZUNGUKO WA KAWAIDA

Ni modeli kielelezo inayokusudiwa kuonyesha kiwango ambacho mfumo changamano ni stahimilivu. Hutumika katika mifumo ya kibiofizikia, mifumo ya kijamii na uchumi, na mifumo ya pamoja ya kibinadamu na asalia. Inajumuisha maarifa kuhusu ukusanyaji wa raslimali au mtaji ndani ya muundo wa mifumo, pamoja na maarifa kuhusu kuongeza uchangamano ambao unatokana na mfuatano wa kiikolojia au utatuzi wa matatizo ya kijamii (Scheffer na wengine, 2002) … Mzunguko wa kawaida unajumuisha awamu ya ukuaji, ukielekea kwa awamu ya kuhifadhi. Msukosuko au msongo, uwe wa kutoka ndani au wa nje, unaweza kusababisha awamu ya mfumuko, na ikiwa hazina ya raslimali iliyopo kwa ajili ya mfumo haijamalizwa na msukosuko, awamu ya mpangilio mpya inaweza kuandaa awamu nyingine ya ukuaji.

The Baltimore Ecosystem Study Urban Lexicon

… awamu hizi nne hazijapangiliwa kwa mstari bali kama mpindo usio na kikomo. Pindi tu shirika lifikiapo awamu ya kilele cha ukuaji (uhifadhi) , linahitaji kuachilia raslimali kwa ajili ya ustawi au mabadiliko na kujiingiza upya katika uvumbuzi ili kudumisha ustahimilivu wake. Awamu ya mfumuko na upangiliaji upya mara nyingi huitwa mpindo wa nyuma, ambapo mabadiliko yasiyo ya kawaida huletwa. Awamu za uvumbuzi na uhifadhi mara nyingi huitwa mpindo wa mbele, ambapo mabadiliko huwa taratibu, na ya kimakusudi zaidi.

Social Innovation Generation, definitions.



Mzunguko wa Kawaida: nadharia ya uhusiano wa mabadiliko katika ustahimilivu katika mifumo changamano.

Chanzo: Ten Conclusions from the Resilience Project. The Resilience Alliance, Peterson, G. (2009).

SWALI OVU

Kifungu maswali maovu matatizo maovu katika njia mahususi ambayo inajumuisha yanayoonekana wakati mitazamo mikubwa miwili kinzani kwa suala hili (ambalo wakati fulani huitwa mtanziko) na kuhitaji ushirikiano na mafikira ya kibunifu.

TATIZO OVU

Matatizo maovu huingia kwa hofu kubwa na huonekana magumu kutatua. Matatizo makubwa katika mifumo changamano ya kawaida kiasilia huwa maovu kwa sababu ya miunganiko, kutokuwa ya moja kwa moja, mipindo ya majibu iliyoimarishwa nk.

Kwa mengi, tazama Dilemmas in a general theory of planning, Rittel na Webber.

UANUWAI

Uanuwai ni sifa kuu katika mifumo changamano na ni muhimu kwa wavumbuzi wa mifumo, ikiwakilishwa katika sekta mbalimbali, stadi nyingi, sehemu nyingi, makundi mengi ya watu nk.

UBADILIKAJI WA MIFUMO

Ni eneo la taaluma ambalo hujumuisha mbinu ya kutengeneza modeli za kompyuta kupata ufahamu na udhibiti mzuri wa mifumo ya kijamii na kimashirika. Hukopa kutoka katika taaluma za mashirika, nadharia maamuzi kuhusu tabia, na uhandisi kutoa msingi wa kinatharia na kivipimo kwa kujenga mahusiano katika mifumo changamano.

The Vocabulary of Systems Thinking: A Pocket Guide, na Colleen Lannon.

UCHANGAMANO

Kuwa na sehemu anuwai zinazojitegemea, lakini zinaingiliana na kutegemeana zilizounganishwa pamoja kupitia kwa miunganiko mingi. Hii ni kinyume kabisa na fikira za moja kwa moja au za kiroboti (wakati mwingine zikiitwa fikira za Kinewton).

UKWATUZI

Imetokana na istilahi ya Kifaransa yenye maana asili ya wakusanyaji wa vyombo chakavu. "Kubuni vitu na kuweka thamani kwa mali ghafi yoyote, haijalishi yalikuwa ya kazi gani mwanzoni."

Social Innovation and Resilience: How One Enhances the Other, F. Westley.

Ufafanuzi mwingine ni: "Uundaji wa kitu bila kutumia chochote: kujenga raslimali kupitia ujasiriamali kwatuzi."

Creating Something From Nothing: Resource Construction Through Entrepreneurial Bricolage, T. Baker na R.E. Nelson.

Ukwatuzi unafahamika kuwa muhimu, kwa kuwa uvumbuzi wa kijamii daima utajumuisha kuunganisha vitu, raslimali au mtaji uliopo.

UMIUNDO

Watu binafsi na miundo hujenga na kuzalisha mifumo ya ikolojia jamii. Ngazi ya chini au ngazi ya jumla haziwezi kufahamika pasipo na nyingine, kwa kuwa hujengana na kuzalishana. Wajasiriamali wa kimifumo hutumia ufahamu huu kuelewa namna uvumbuzi wao wa kijamii unawezaje kujengwa na ngazi na jinsi gani wanaweza pia kuwa wanazalisha hali chanya au hasi za mifumo iliyopo.

UPEO

Kwa jumla huchukuliwa kama kinyume na jadi, ufafanuzi wa mifumo kimsonge, upeo hurejelea aina ya hali ya ikilojia-jamii ambayo *inaingiana na kusukana* na hujumuisha mabadiliko ya mzunguko wa kawaida katika kila kiwango, na maingiliano baina ya viwango.

Panarchy: Theory and Application, Craig R. Allen, na wengine.

Katika hili kuna wazo la viwango vya misuko: mifumo hupatikana katika viwango tofauti ambavyo huingiliana sana, na ambavyo hupitia mizunguko katika nyakati na kasi tofauti. Mizunguko ya kawaida "imesukana, mmoja ndani ya mwingine, ndani ya viwango vya nafasi na wakati," (Holling, na wengine, 2002) na kwa hivyo, mabadiliko katika hatua moja huweza kuathiri hatua nyingine.

Mengi, tazama When scaling out is not enough: strategies for systems change, Westley na Antadze, 2013.

USTAHIMILIVU

Ni uwezo wa kupokea vishindo huku ukiendelea kuzoea, kujifunza na kubadilika.

Handbook of Sustainability and Social Science Research.

Ustahimilivu haupendelewi mara zote; wakati fulani wajasiriamali wakimifumo huhitaji kujitahidi kupunguza ustahimilivu wa mifumo iliyokita.

UVUMBUZI WA KIJAMII

Ni mawazo mapya, matendo, programu, michakato au bidhaa mpya ambazo hubadilisha mtiririko wa rasilimali na mamlaka katika kiwango kipana cha mifumo ya kijamii na kiikolojia. Hili linahusisha mikakati ya maingiliano kati ya wajasiriamali wa kijamii na wa kiasasi wanaopatikana katika ngazi mbalimbali kutoka katika jamii hadi kwa asasi pana za kisiasa, kichumi, na kitamaduni ambazo huunda jamii zetu.

UVUMBUZI WA MIFUMO

Ni mabadiliko katika kiwango kipana cha mfumo wenyewe; sio kusaidia mfumo uzoee, Bali kuusaidia ubadilike, yaani, kubadilisha ruwaza za maana na mienendo ambayo huchonga maingiliano ya kijamii kwa muda; kubadilisha ruwaza za kimsingi za kijamii za kanuni, imani, miundo ya utawala, msambao wa raslimali, nk., mambo ambayo mwanzo huchangia kuwepo kwa matatizo.

VIPENGELE VYA MIFUMO

Mifumo hujengwa na vifaa, sifa, mahusiano na mazingira. Unapotafiti mfumo, umuhimu upo katika mahusiano na utegemeanaji wa vipengele, badala ya kipengele kimoja kimoja.

Schwab Foundation, Social entrepreneurs and systems change, 2017.

VIWANGO Mifumo hufanya kazi katika viwango mbalimbali: watu binafsi, familia, ujirani, miji, mataifa, na jamii ya ulimwengu.

Katika uvumbuzi wa kijamii, maneno ngazi na kueneza hutumika. Ngazi za kijamii na ikolojia jamii huhusisha viwango mbalimbali. Kiwango cha jumla kinabainishwa na kaida, imani, thamani, imani za kiroho, na mienendo mikuu ya kijamii, kiikolojia, kiuchumi na kiteknolojia. Ngazi za viwango vya kati hujumuisha seti muhimu za lugha na utawala ambazo hubaini ni nani ana uwezo, ni jinsi gani raslimali husambaa, na miundo mikuu ya mashirika ambayo huchonga uongozi na sera. Ngazi za viwango vya chini ngazi huhusisha maingiliano ya watu binafsi na huweza kuhusisha mazingira finyu ya kujaribia uvumbuzi.

Mengi, tazama Scaling Out, Scaling Up, Scaling Deep: Advancing Systemic Social Innovation and the Learning Process to Support It, Darcy Riddell na Michele-Lee Moore.